

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Baruapepe:info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz



Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
Jengo Na. 10,
S. L. P. 10,
40479 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CHA-281/360/01D/48

29 Novemba, 2017

Katibu Mtendaji,
Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),
S.L.P. 6562,
DAR ES SALAAM.

Katibu Mtendaji,
Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE),
S.L.P. 7109,
DAR ES SALAAM.

**Yah: VYUO VIKUU KURUHUSIWA KUTOA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI
YA ASTASHAHADA NA STASHAHADA KWA WALIMU WALIO KAZINI**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Mwaka 2016 Wizara ilitoa Waraka wa Elimu Na. 5 uliohusu Mwongozo wa Utekelezaji wa Programu za Mafunzo ya Ualimu. Mojawapo ya maelekezo ya Waraka huu yalikuwa ni kuweka usimamizi wa mafunzo ya Walimu Tarajali chini ya usimamizi wa Kamishna wa Elimu.

Wizara imepata maombi ya baadhi ya Vyuo Vikuu ambavyo vilikuwa vinatoa mafunzo ya Ualimu pamoja na programu nyingine kuomba kuruhusiwa kuendelea kutoa mafunzo hayo ya Ualimu katika Ngazi za Astashahada na Stashahada.

Wizara imepitia maombi hayo na kutambua kwamba; Vyuo Vikuu vina mfumo wake madhubuti wa Uhakiki na Uthibiti wa Programu wanazotoa na vilevile Programu za Mafunzo ya Stashahada na Astashahada katika Vyuo Vikuu zinadahili walimu walio kazini.

Hivyo basi, Vyuo Vikuu vijulishwe kuendelea na utaratibu wa kutoa Elimu ya Ualimu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada, kwa walimu walioko kazini. Mafunzo Tarajali ya Ualimu yataendelea kusimamiwa na kuratibiwa na Wizara kupitia Ofisi ya Kamishna wa Elimu.

Nakutakieni kazi njema.



Dkt. Leonard D. Akwilapo
KATIBU MKUU